**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA 01 CHA BODI YA WAMACU LTD KILICHOFANYIKA TAREHE 13/04/2023 KATIKA OFISI ZA WAMACU LTD TARIME MJINI, KUANZIA SAA 09:30AM AHSUBUHI.**

- **Mahudhurio**

**WAJUMBE & KATIBU WA BODI YA WAMACU LTD**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | David Mwita Hechei | - | M/kiti wa Bodi |
| 2. | Samwel Gisiboye Marwa | - | Katibu |
| 3. | Michael Joseph Mugwewa | - | M/M/Kiti |
| 4. | Elius Marwa Samwel | - | Mjumbe |
| 5. | Momanyi Range | - | Mjumbe |
| 6. | Kurwa Nyamohanga Mwita | - | Mjumbe |
| 7. | Julius Makonyo Makara | - | Mjumbe |
| 8. | Emmanuel Ndege Bensoni | - | Mjumbe |
| | **MJUMBE MKARIBISHWA.** | | |
| 9. | James Marwa Makorom | - | Mwakilishi wa Wakulima |
| 10. | Ibrahim H. Nsumiyinda | - | Mhasibu ofisi ya RPC Tarime Rorya |

**<u>AGENDA</u>**

1. Kufungua kikao
2. Kuomba UWAKALA wa NMB katika Benki ya NMB tawi la Tarime;
3. Kutekeleza **AG.NA.7 AZIMIO NA.11** la Mkutano Mkuu wa 13 la kuwasilisha Makisio ya Mapato na matumizi pamoja na Ukomo wa Madeni kwa MRAJISI kwa ajili ya kuidhinishwa;
4. Kuomba kuwekewa fedha ya mkopo kiasi cha TZS bilioni tatu na milioni mia tano tu (3,500,000,000/=); na
5. Kufunga kikao.

**AG.Na.01/4: KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu wa kikao alisimama na kuwasalimia wajumbe wa kikao kwa salamu ya ushirika, na baada ya salamu aliwafahamisha wajumbe kuwa hiki ni kikao cha dharura cha 01 cha Bodi ni kwa ajili ya kuomba uwakala wa Benki kwa ajili ya kuthibiti mauzo ya mbolea yanayofanyika yanayofanywa na chama kila siku; na baada ya kusema hayo alimkaribisha M/kiti wa BODI **Ndg. David Hechei** kufungua kikao.

**M/kiti Ndg. David Hechei,** alisimama na kufungua kikao mnamo saa tatu (10:10am) ahsubuhi kwa kuwasalimia wajumbe na kabla ya kuanza AGENDA za kikao M/kiti amemtambulisha **Ndg Ibrahimu H. Nsumiyinda, Mhasibu** wa **Ofisi ya Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya** ambaye amefika hapa ofisini kwa swala maalumu. Aidha alimwomba kuwasalimia wajumbe na kusema Jambo Lake.

**Afande Ibrahimu, Mhasibu** aliwasalimia wajumbe na kuishukuru Bodi kumpa nafasi hii adimu kushiriki naye katika kikao chao, na kusema kuwa imekuwa vizuri zaidi kuikuta Bodi na swala lake linaweza kueleweka kwa haraka sana. Baada ya hapo aliwaeleza wajumbe kuwa **RPC** alihitaji kuwalipa kodi ya pango kwa kipindi hiki hadi mwezi wa sita kwa gharama ya zamani ili kuepuka hatari ya kurudishwa kwa fedha kabla mwaka wa fedha haujafungwa Juni, 30.

Wajumbe kwa waliona jambo hili kuwa ni jema na kwa pamoja walilikubali kuwa lifanyike kwa busara hiyohiyo ili taratibu zingine hizo zitakamilishwa hapo baadaye ikiwa kama **Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Tarime-Rorya** atahitaji kuendelea kulitumia jengo hilo. Baada ya maelezo hayo M/kiti aliipongeza ofis ya Kamanda kwa hatua hiyo na kuwajulisha kuwa bado sisi kama WAMACU LTD tunapenda waendelee kuwepo na hata kwetu ni usalama zaidi katika shighuli zetu. Baada ya kusema hayo alifungu kikao na kumwomba katibu kusoma AGENDA inayofuata.

**AG.NA.02/4: KUOMBA UWAKALA WA NMB KATIKA BENKI YA NMB TAWI LA TARIME**

Katibu alisoma AGENDA hii na badaye kumruhusu M/kiti kuendelea na mjadala wa wajumbe; na kuomba katibu atoe ufafanuzi zaidi juu ya AGENDA hii na inalenga nini kwenye ushirika wetu wa WAMACU LTD. Katibu aliwaeleza wajumbe wa kikao kuwa katika mradi wa mbolea unaoendelea hapa WAMACU tunaweza kuuza mbolea zaidi ya mifuko mia nane ambayo hiyo ni sawa milioni arobaini na tano (45,000,000) kwa siku.

Pia kupitia Ofisi ya Mrajisi Mkoa wa Mara tumepokea WARAKA WA AGIZO LA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA la kutvitaka vyama vyote vya ushirika kuwa MAWAKALA wa MABENKI; na hivyo sisi WAMACU kupitia uongozi, menejimenti na Benki ya NMB tumejadiliana tukaona ni vema kuwa na WAKALA atakayeratibu biashara na mauzo ya fedha za PEMBEJEO za kilimo hasa (mbolea) inayoendela hapa ofisini kwa sasa.

Hata hivyo UWAKALA ni biashara kama zilivyo biashara zingine, zina faida ikiwa kuna mzunguko wa fedha yaani (cashflow) katika eneo linahusika na utoaji wa huduma hiyo. Kwa bahati nzuri pia Benki imekubali kuipa WAMACU uwakala huu katika kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma kwa mkulima unakuwa mwepesi.

Wajumbe baada ya kupokea maelezo ya katibu, wote kwa pamoja walikubaliana na kuagizi utekelezaji wa maombi hayo kufanyika haraka kwa ajili ya UWAKALA. Pia walisisitiza kuwa ni jambo jema la kuomba uwakala na kusisitiza sana juu ya umakini katika shughuli hii na uaminifu mkubwa ili kuhakikisha kuwa fedha inaingia ndani.

Pia Mr Ibrahim amepongeza Bodi ya chma na kuwatakia kazi njema hasa kwa kitendo cha kukubali ombi la ofisi yake, aidha amesisitiza sana juu ya umakini kwenye hela inayokusanywa taslimu pamoja na huo uwakala tunaoenda kuchukua kutoka Benki. Pia Ibrahim aliwaisihi wajumbe wa Bodi kuomba

RPC usalama kwa ajili shughuli hiyo ikiwezekana hasa pale atakapokuwa ameondoa makazi ya ofisi yake eneo hili.

Pia wajumbe kwa kutambua kuwa hii ni account, kama zilivyo zingine wameteua watia saini wawili wawili kutoka kila kundi; na baada ya hapo wametoa maazimio kama ifuatavyo:-

**MAAZIMIO.**

1. Wajumbe wameazimia kuomba UWAKALA wa Benki ya NMB kwa ajili ya kuratibu shughuli zake za pembejeo hapa WAMACU LTD Tarime Mjini;
2. Pia wajumbe wameazimia kuhusu watia saini kama ifuatavyo:-
   **KUNDI A:** WATUMISHI

   1. Mohamed Sakilu - Mhasibu Msaidizi
   2. Olais Piniel - MENEJA SHUGHULI& BIASHARA

   **KUNDI B:** WAJUMBE WA BODI

   3. Elius Marwa - Mjumbe wa BODI
   4. Michael Joseph Mughwewa- Makamu M/kiti wa BODI
3. Aidha wajumbe wameazimia kuwa fedha itatolewa na mmoja kwa kila kundi, kama itakavyofafanuliwa kwenye barua ya kuomba kufungua akaunti ya UWAKALA.
4. Pia waliazimia kuwa kila mwamala wa malipo uuonekane kupitia akaunti MENEJA MKUU ili kuongeza uthibiti.

**AG.Na.03/4: KUTEKELEZA AG.NA.7 AZIMIO NA.11 LA MKUTANO MKUU WA 13 LA KUWASILISHA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI PAMOJA NA UKOMO WA MADENI KWA MRAJISI KWA AJILI YA KUIDHINISHWA.**

Katibu amesoma AGENDA hii na kuifafanua zaidi kuwa makisio hayajawasilishwa kutokana na kuchelewa kwa chama chetu kusajiriwa kwa njia ya mfumo, aidha baada ya kuwa tumesajiliwa sasa ni wakati mwafaka wa kutekeleza AZIMIO la Mkutano Mkuu wa 13 uliofanyika tarehe 27/01/2023. Wajumbe kwa pamoja walikubalina na katibu na kuazimia kuwa hilo ni swala la utekelezaji wala halihitaji kujadiliwa tena zaidi.

**AZIMIO.**

1. Wajumbe kwa pamoja wameazimia kuwa utekelezaji ufanyike kwa makiso ya mapato na matumizi pamoja na ukomo wa madeni kuwasilishwa kwa Mrajisi kwa ajili ya kuidhinishwa.
2. Aidha wajumbe wameazimia swala hilo kufanyika kwa njia ya mfumo kama ilivyoagizwa na Mrajisi Taifa.

**AG.Na.04/4: KUOMBA KUWEKEWA FEDHA YA MKOPO KIASI CHA TZS BILIONI TATU NA MILIONI MIA TANO TU (3,500,000,000/=).**

Katibu alisoma AGENDA hii na kuwaomba wajumbe wapitishe maombi ya mkopo wa fedha ya kukusanyia kahawa kutoka **Benki ya Kilimo "TADB"**. Fedha hiyo ilipitishwa na **Mkutano mkuu wa 13** uliofanyika tarehe **27/01/2023** katika ukumbi wa **Blue Sky**, **AG.Na.14, AZIMIO Na.1** kuwa chama kiwasilishe maombi haya ya mkopo haraka ili wakulima waweze kupata fedha ya kukusanyia kahawa.

Wajumbe wote kwa pamoja waliunga mkono hoja hii na kupitisha kuwa maombi haya yawasilishwe haraka sana Benki baada ya kuwa chama kimepata offer ya mkopo huo. Aidha walipitisha jumla ta TZS bilioni tatu na milioni mia tano tu (**3,500,000,000/=**) kama ilivyowasilishwa kwenye ombi la awali.

**MAAZIMIO**

1. Wajumbe kwa pamoja wamepitisha maombi ya **TZS bilioni 3,500,000,000/=** kwa ajili ya kukusanyia kahawa ya wakulima.
2. Aidha wameazimia kuwa offer ikitoka barua iandikwe haraka sana kwa ajili ya fedha hiyo ili iwekwe mapema kwa kazi hiyo.

**AG.Na.05/4: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti Ndg. David Hehei, alisimama na kuwashukuru wajumbe wote wa BODI kwanza kwa kukubali kujadili AGENDA hii muhimu ya kikao cha dharura na kutoa michango yao iliyowezesha jambo hili kufanikiwa na hatimaye kuruhusu menejimenti kuwasilisha maombi haya Benki. Pia aliwapongeza kwa uvumilivu na ushirikiano wao kwani kikao hiki kilikuwa cha dharura sana. Baada ya kusema hayo aliahirisha kikao mnamo saa 10:25 ahsubuhi na kuwatakia safari njema wajumbe waendapo majumbani mwao hadi hapo kikao kitakapoitishwa tena.

***Muhtasari huu umesainiwa kwa niaba ya wajumbe BODI na***

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

TAREHE……………………………………